# Daima Tunakumbushwa kuungama dhambi zetu hata kama ni ndogo kiasi gani

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · December 20, 2016

Makala za Tafakari Kwa Wakatoliki · #Karibu AckySHINE · #Tafakari za Toba na Msamaha

Kulikuwa na vijana wawili walioamua kwenda kwa padri kumwelezea shida zao. Basi walipofika kwa yule padre, wakamwambia padre, " samahani padre tuko hapa mbele yako kwa kuwa tumejisikia kuwa ni wadhambi ha hivyo tunahitaji kuungama.

Basi wakwanza akamwambia padre, " Mimi dhambi zangu ni kubwa sana hata ninaona aibu kuziungama", wa pili akamwambia padre, " sahamani padre mimi nimetenda dhambi ila siyo kubwa sana kama za mwenzangu, bali ni dhambi ndogondogo." Baada ya kusikia hayo padre aliwaambia basi kila mmoja aende akaokote mawe kadiri ya dhambi alizozitenda na akamletee. Hao vijana walienda kuokota mawe kadiri ya dhambi za kila mmoja wao. Mmoja wao alileta jiwe moja kubwa ambalo alikuja akilivilingisha hadi pale alipokuwepo padre, na mwingine alileta mawe madogomadogo mengi kwenye mfuko. Baada ya padre kuone kuwa walifanya alivyowaagiza, basi aliwaambia kuwa kila mmoja arudishe mawe yake sehemu ile ile alipoyaokota. Yule aliyebeba jiwe kubwa ilikuwa rahisi kujua alipolitoa hivyo alilivilingisha mara moja na kulirudisha mahali pake, wakati yule aliyekuwa na mawe madogomadogo alishindwa kukumbuka mahali alipoyatoa, hivyo akaishia kuhangaika na kumwambia padre kuwa hawezi kumbuka mahali alipotoa kila jiwe, na kwake ni vigumu.

Baada ya hayo padre aliwaambia wote kuwa yule mwenye dhambi kubwa daima ni rahisi kuiungama maana huwa inashika nafasi kubwa katika nafsi yake na inamfanya asiwe na amani daima, kwa hivyo ni rahisi kukumbuka kuiungama dhambi yake, vilevile padre akamgeukia yule mwingine aliyebeba mfuko wa mawe madogomadogo na akamwambia kuwa, jinsi ulivyoshindwa kurudisha hayo mawe katika nafasi yake kila moja, ndivyo ilivyo kwa dhambi ndogondogo ulizotenda. Dhambi zionekanazo kuwa ni ndogo zaweza sahulika na kukufanya utende dhambi nyingine ya kutokukumbuka wajibu wako wa kuungama ukidhani kuwa hujatenda dhambi.

Daima tunakumbushwa kuungama dhambi zetu hata kama ni ndogo au hata kama tumesahau, kwa maana kuna zile dhambi ambazo ni nyepesi na rahisi kusahulika na hivyo kutufanya daima tujihisi kuwa sisi hatuna haja ya kuungama.